# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA

# SAYANSI

## KWA SKULI ZA MSINGI

## DARASA LA I –IV

**2009**

**© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2009**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kutoa muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**UMETAYARISHWA NA:**

**IDARA YA MITAALA NA MITIHANI**

**S.L.P. 3070**

**ZANZIBAR**

## YALIYOMO

**Ukurasa**

**UTANGULIZI** ... v
Sababu za kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi ... v
Umuhimu wa Somo la Sayansi ... vi
Madhumuni ya Elimu Zanzibar ... vii
Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi ... vii
Ujuzi wa Jumla katika Somo la Sayansi ... viii
Malengo ya Jumla ya Somo la Sayansi ... ix
Uchaguzi na Mpangilio wa Mada ... ix
Muundo wa Muhtasari ... xi
**DARASA LA KWANZA** ... 1
UJUZI ... 1
MALENGO ... 2
**DARASA LA PILI** ... 30
UJUZI ... 30
MALENGO ... 31
**DARASA TATU** ... 55
UJUZI ... 55

MALENGO ........................................................................ 56
**DARASA LA NNE** ........................................................................81
UJUZI ........................................................................ 81
MALENGO........................................................................82

## UTANGULIZI

Muhtasari huu ni wa somo la Sayansi ambalo katika mtaala mpya (2009) litafundishwa katika Darasa la I hadi la IV. Katika mtaala wa 1998, ambao umedumu hadi 2009, mada za somo la Sayansi zilikuwa zikifundishwa tangu Darasa la I hadi III katika somo la Mazingira na Darasa la IV - VII katika somo la Sayansi. Utangulizi huu una maelezo kuhusu sababu za kuandika mtaala mpya na umuhimu wa somo la Sayansi katika mtaala wa elimu ya Msingi. Hii inafuatiwa na Madhumuni ya Elimu Zanzibar na Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar. Vile vile, kuna orodha ya ujuzi na malengo ya jumla ya somo yakifuatiwa na maelezo kuhusu uchaguaji na mpangilio wa mada. Mwisho, kuna maelezo kuhusu yaliyomo katika safu-wima za jadweli za ufundishaji na ujifunzaji.

### Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi.

Mnamo mwaka 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendesha mchakato wa kufanya mapitio, kufupisha na kuandika upya mtaala wa elimu ya msingi. Madhumuni yalikuwa ni kufanya mtaala ushabihiane na Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006). Sera hii inalenga kurekebisha ubora na muundo wa elimu ya msingi pamoja na kuweka muunganiko bayana kati ya elimu ya maandalizi, msingi na sekondari ili kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Sera ya Elimu ya 2006 imebadili muundo wa elimu kwa kutamka kuwa elimu ya maandalizi itakuwa ni sehemu ya elimu ya lazima, elimu ya msingi itakuwa ni ya miaka sita (6) badala ya saba (7) na baadhi ya masomo ya ngazi ya msingi yatafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa madarasa ya Tano na Sita.

Mambo mengine yaliyochochea mapitio haya ni pamoja na:

- Mwelekeo wa kilimwengu katika maendeleo ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia.
- Mwitiko wa serikali kwa Wazanzibari kudai nafasi zaidi za skuli kwa watoto wote na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa.
- Mwitiko wa serikali kwa matokeo ya Utafiti wa Mahitaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi wa 2008.

Utafiti wa 2008 ulizingatia mapungufu yafuatayo katika mtaala wa 1998:

Haukukuza stadi za kuwasiliana, ubunifu na fikra yakinifu.

Haukuzingatia vya kutosha mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na masuala mtambuka.

Ulihimiza matumizi ya mbinu za kufundishia/kujifunzia zilizojikita kwa mwalimu zaidi kuliko kwa mwanafunzi.

Ufundishaji/ujifunzaji ulikuwa wa kinadharia zaidi kuliko kuwa wa vitendo au ushiriki wa wanafunzi.

Kutokana na changamoto hizo serikali iliamua kufanya yafuatayo:

- Kutoa elimu ya msingi inayojikita katika vitendo vya wanafunzi na ukuzaji wa stadi, maarifa na mwenendo.
- Kuweka muunganiko bayana kati ya mtaala wa elimu ya maandalizi, msingi na sekondari ili kuepukana na tatizo la mada kurudiwa rudiwa.

**Umuhimu wa Somo la Sayansi**

Sayansi huwezesha wanafunzi kujifunza kupitia uchunguzi na udadisi. Hivyo, wanapata mwelekeo, maarifa na stadi za kisayansi kupitia vitendo vyao vya siku hadi siku wawapo nyumbani au skuli. Wanafunzi hutumia maarifa na stadi za sayansi na teknolojia kuchunguza na kutambua uhusiano kati ya mambo kama afya na lishe, mashine na urahisishaji wa kazi, rutuba na uzalishaji wa mazao bora. Kwa hiyo, kujifunza sayansi huwezesha wanafunzi kuelewa mazingira yanayowazunguka. Maarifa, stadi na mwelekeo waupatao huwawezesha kung'amua kwamba matatizo yanaweza kutatuliwa. Huwawezesha kutafuta taarifa, kufanya majaribio ya mawazo yao na kuwa wabunifu.

**Madhumuni ya Elimu Zanzibar**

Yafuatayo ndiyo madhumuni na malengo ya elimu Zanzibar:

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo/mwenendo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, pamoja na haki, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.
5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

**Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi**

Yafuatayo ndiyo madhumuni na malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar:

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.
2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.

3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha miongoni mwa wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na ya wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi, fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi na ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu na mataifa mengine.
11. Kuwezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na ufahamu wa hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.
12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi kwa mazingira wanamoishi pamoja na utashi wa kuyatunza.

**Ujuzi wa Jumla katika Somo la Sayansi**

Mtaala huu umejikita katika kumpatia ujuzi mwanafunzi (badala ya kujikita katika kufundisha/kujifunza maudhui tu). Ujuzi ni muunganiko sawia wa maarifa, stadi na mwenendo/mwelekeo anavyotarajiwa kuvipata mwanafunzi. Hivyo, baada ya kusoma somo la Sayansi hadi Darasa la IV wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kuchunguza, kuainisha na kutekeleza mahitaji ya afya ya binadamu.
2. Kuainisha na kueleza tabia na sifa za viumbe hai na visivyo hai.
3. Kupenda na kutumia stadi, maarifa, kanuni na dhana za kisayansi katika maisha ya kila siku.
4. Kuainisha mambo yanayoharibu mazingira na kujiepusha nayo.
5. Kutumia stadi za kupata maarifa ya kisayansi kupitia maktaba na vifaa viyengine vya TEHAMA. .(Teknolojis ya Habari na Mawasiliano)

**Malengo ya Jumla ya Somo la Sayansi**

Somo la Sayansi linafundishwa katika skuli za msingi ili wanafunzi waweze:

1. Kujenga tabia ya utumiaji wa stadi, maarifa, kanuni na dhana za kisayansi katika maisha ya kila siku.
2. Kutambua tabia na sifa za viumbe hai na visivyo hai.
3. Kutambua mifumo ya miili yao na mahitaji ya afya ya mwili.
4. Kutumia stadi za kupata maarifa ya kisayansi kutoka maktaba na vifaa vyengine vya TEHAMA.(Teknolojis ya Habari na Mawasiliano)

**Uchaguzi na Mpangilio wa Mada**

Muhtasari huu umeundwa kwa mfuatano wa mada za sayansi, kila moja ikiwa na mada ndogo kadhaa. Hizi zimepangwa makusudi ili maarifa na stadi zitakazopatikana katika darasa moja ziwe msingi wa kujifunza mada ndogo za darasa linalofuata. Vile vile, kuna mada zinazohusu masuala mtambuka kama madawa ya kulevya, mazingira, teknolojia ya habari na mawasiliano, ujasiriamali na stadi za maisha,hususani msongo na namna ya kuuhimili. Mwalimu anashauriwa kufundisha mada hizi kwa mfuatano uliopo kwenye muhtasari. Zifuatazo ndizo mada zilizochaguliwa na kusambazwa katika madarasa ya I – IV.

| NA. | MADA KUU | DARASA 1 | DARASA II | DARASA III | DARASA IV |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Usafi. | √ | √ | √ | √ |
| 2. | Afya ya Mwili. | √ | √ | √ | √ |
| 3. | Chakula na Lishe. | √ | √ | √ | √ |
| 4. | Huduma ya Kwanza. | √ | √ | √ | √ |
| 5. | Wanyama. | √ | √ | √ | √ |
| 6. | Ndege. | √ | √ | - | - |
| 7. | Wadudu. | √ | √ | - | - |
| 8. | Mimea. | √ | √ | √ | √ |
| 9. | Misitu. | - | - | - | √ |
| 10. | Maji. | √ | √ | √ | √ |
| 11. | Hewa. | √ | - | - | - |
| 12. | Udongo. | - | √ | √ | - |
| 13. | Mwanga. | √ | √ | √ | √ |
| 14. | Sauti. | √ | √ | √ | √ |
| 15. | Joto. | √ | √ | √ | √ |
| 16. | Umeme. | √ | √ | √ | √ |
| 17. | Sumaku. | - | - | √ | √ |
| 18 | Stadi za kazi. | √ | √ | √ | √ |

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za Mwanzo na Jadweli za Ufundishaji/Ujifunzaji.

**Kurasa za Mwanzo**

Sehemu hii inajumuisha jalada la muhtasari, ukurasa wa jina la muhtasari, ukurasa wa haki-miliki na wa yaliyomo. Vilevile, kuna taarifa kuhusu sababu za kuandika mtaala mpya , Madhumuni ya Elimu Zanzibar na Malengo ya Elimu ya Msingi. Kurasa zinazofuata zinaonesha ujuzi wa jumla katika somo la sayansi, malengo ya jumla ya somo na taarifa kuhusu mpangilio wa mada.

**Jadweli ya Ufundishaji na Ujifunzaji**

Sehemu hii imegawika katika maeneo manne, kila moja likiwakilisha darasa moja (Darasa la I hadi IV). Muhtasari wa kila darasa unatanguliwa na orodha ya ujuzi wa jumla na malengo ya jumla ya darasa husika. Kisha linafuata jadweli lenye safu-wima sita zenye vichwa vya: mada kuu/mada ndogo; malengo mahsusi; mbinu za kufundishia/kujifunzia; vifaa/zana; upimaji na vipindi. Yafuatayo ni maelezo ya kila kipengele.

***Mada kuu/Mada ndogo***

Mada hutamka maudhui yatakayofundishwa. Chini ya mada kuna mada ndogo ambazo huonesha kina na mawanda ya ufundishaji/ujifunzaji wa mada husika.

***Malengo mahsusi***

Kila mada ndogo imeandikiwa lengo au malengo mahsusi. Hayo yanaeleza stadi, mwenendo/mwelekeo na maarifa ambayo kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo husika. Malengo mahsusi ndiyo yanatumiwa kufanyia upimaji. Aidha, ufikiaji wa malengo mahsusi katika kujifunza hutafsiriwa kama ufikiaji wa stadi, mwelekeo na maarifa yanayolengwa katika mada husika. Kila mwanafunzi katika darasa anatakiwa kuyafikia malengo mahsusi yaliyotajwa . Hivyo, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa lugha ya alama inatumika kumfundisha mwanafunzi kiziwi, na mashine ya Braille au zana mguso zinatumiwa kwa mwanafunzi asiyeona. Kwa ajili ya makundi mengine ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, taratibu, miongozo, vifaa na mbinu za kufundishia/kujifunzia zinazostahiki zitumike ipasavyo.

***Mbinu za kufundishia/kujifunzia***

Safu - wima hii inaonesha baadhi ya mbinu zinazofaa kufundishia/kujifunzia. Ni mbinu shirikishi tu zinazopendekezwa kwa sababu zinahimiza wanafunzi kujitafutia maarifa na kujenga maana kwa kile wanachojifunza. Mbinu hizo ni kama vile majadiliano ya vikundi; maigizo; nyimbo, michezo, changanyakete; bungua-bongo; ziara za kielimu, kumwalika mgeni na nyingine ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kutegemea mazingira, mada na umri wa wanafunzi. Mbinu zilizomo katika safu - wima hii ni mapendekezo tu. Mwalimu anashauriwa atumie mbinu nyengine anazozimudu zitakazoshirikisha wanafunzi na kufanikisha ufundishaji/ujifunzaji.

***Vifaa/Zana***

Safu- wima hii imesheheni mapendekezo ya zana na vifaa ambavyo vinafaa kutumiwa katika kufundisha/kujifunza kila mada. Mwalimu anashauriwa kuzitumia hizi pamoja na nyengine atakazoona zinafaa au zinapatikana katika mazingira yake. Vile vile mwalimu anashauriwa

kubuni na kutengeneza zana/vifaa kulingana na upatikanaji wa malighafi katika mazingira yake. Aidha, wanafunzi wahimizwe kubuni na kutengeneza zana za kufundishia/kujifunzia kwa kutumia mahitaji za bei nafuu zinazopatikana katika mazingira yao.

***Upimaji***

Safu –wima hii inaonesha maelekezo ya upimaji wa wanafunzi. Inampasa mwalimu kupima maendeleo ya kila siku ya wanafunzi wake. Hii itamwezesha kujua uwezo na matatizo ya wanafunzi, ubora wa mbinu za kufundishia/kujifunzia anazozitumia na ubora wa zana/vifaa anavyotumia. Vile vile, upimaji humwezesha mwalimu kupanga na kutekeleza mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wazito. Aidha, upimaji humwezesha mwalimu kupendekeza marekebisho ya mtaala na vitabu vya kufundishia/kujifunzia. Upimaji wa mwisho wa muhula au mwaka huonesha kiwango cha ujuzi alichofikia mwanafunzi. Kwa sababu hizo, mwalimu anashauriwa kupima maendeleo ya mwanafunzi kila siku anapofundisha, kila mwezi, kila muhula na kila mwaka kwa kuzingatia malengo mahsusi ya kila mada iliyofundishwa na njia mwafaka za upimaji.

***Vipindi***

Safu –wima hii inaonesha idadi ya vipindi vilivyokadiriwa kufundisha kila mada. Makadirio hayo yanafikiwa kwa kujumlisha idadi ya vipindi vya siku 224 za mwaka wa masomo na kuvigawa kwa idadi ya mada ndogo zilizomo katika muhtasari. Tofauti ya idadi ya vipindi baina ya mada ndogo imezingatia kina cha mada ndogo na idadi ya malengo mahsusi yanayoihusu. Hata hivyo, mwalimu anaweza kurekebisha mgawanyo wa idadi ya vipindi kwa mada ndogo kwa kutegemea mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wake. Utawala wa skuli unahimizwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura za sikukuu za kidini au za kiserikali.

Somo la Sayansi lina vipindi vinne (4) kwa wiki kwa Darasa la I – IV. Muda wa kipindi kimoja kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi ni dakika 40 kwa shifti ya asubuhi; ni dakika 35 kwa shifti ya mchana. Siku za Ijumaa muda wa kila kipindi utakuwa dakika 30 tu.

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**ZANZIBAR**

## DARASA LA KWANZA

**UJUZI**

Baada ya kusoma somo la Sayansi katika Darasa la I wanafunzi wataonesha ujuzi wa :-

1. Kuweka mwili na mavazi katika hali ya usafi.
2. Kutumia na kuhifadhi vyakula ipasavyo.
3. Kuainisha na kujikinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza.
4. Kueleza na kutoa Huduma ya Kwanza kwa usahihi.
5. Kuainisha na kueleza wanyama na sifa zao.
6. Kuainisha na kutumia kwa njia endelevu vyanzo vya maji na hewa.
7. Kuainisha na kueleza vyanzo asili na visivyo asili vya nishati anuai.
8. Kuainisha na kutumia stadi za kazi anuai.
9. Kutumia maktaba na vifaa vyengine vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kisayansi.
10. Kusafisha na kutunza mazingira yao.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Sayansi katika Darasa la I ni kuwezesha wanafunzi:-

1. Kutambua dalili na njia za maambukizo ya magonjwa ya kuambukiza(yaliyoainishwa) na kujiepusha nayo.
2. Kutambua umuhimu wa usafi wa mwili na mavazi pamoja na utekelezaji wake.
3. Kutambua uhifadhi na matumizi ya vyakula ipasavyo.
4. Kutambua aina za wanyama, tabia na vyakula vyao.
5. Kuelewa aina za mimea na sifa zake.
6. Kutambua vyanzo vya hewa na maji, umuhimu na matumizi yake endelevu.
7. Kufahamu utoaji wa Huduma ya Kwanza kwa usahihi.
8. Kufahamu umuhimu na matumizi ya vyanzo vya asili na visivyo vya asili vya nishati anuai.
9. Kutambua aina za stadi ya kazi na matumizi yake.
10. Kufahamu matumizi ya maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kisayansi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. USAFI<br>a) Vifaa vya Usafi wa Mwili na Mavazi. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kutaja aina mbalimbali za vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba wimbo wa vifaa vya usafi wa mwili na mavazi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | 1. Chati ya wimbo wa usafi wa mwili na mavazi.<br>2. Chati/Picha za vifaa vya usafi wa mwili na mavazi.<br>3. Chati mguso ya wimbo wa usafi wa mwili.<br>4. Chati/Picha mguso ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja aina mbalimbali za vifaa vya usafi wa mwili na mavazi? | 10 |
| | (ii) Kuchora baadhi ya vifaa vya usafi. | Kwa kutumia mbinu ya kuchora, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchora baadhi ya vifaa vya usafi. | 1. Picha za baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi.<br>2. Picha mguso za baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi? | |

| MADA KUU/ MADANDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kutumia baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi. | 1. Ndoo.<br>2. Beseni.<br>3. Taulo.<br>4. Dawa ya meno.<br>5. Mswaki.<br>6. Kiwembe/mkasi.<br>7. Dodoki.<br>8. Sabuni.<br>9. Maji.<br>10. Soksi.<br>11. Brashi.<br>12. Rangi ya viatu. | Je, mwanafunzi anaweza kutumia baadhi ya vifaa vya usafi wa mwili na mavazi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Usafi wa Mwili. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kutaja sehemu mbalimbali za mwili zinazohitaji kufanyiwa usafi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo inayotaja sehemu za mwili zinazohitaji usafi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja sehemu za mwili zinazohitaji usafi. | 1. Chati ya wimbo inayohusu sehemu za mwili wa binadamu.<br>2. Chati inayoonesha sehemu za mwili wa binadamu.<br>3. Chati mguso ya wimbo inayohusu sehemu za mwili wa binadamu.<br>4. Chati mguso inayoonesha sehemu ya mwili wa binadamu. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja sehemu mbalimbali za mwili zinazohitaji kufanyiwa usafi? | 10 |
| | (ii) Kutaja faida za usafi wa mwili. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awongoze wanafunzi kueleza faida za usafi wa mwili. | 1. Chati inayoonesha faida za usafi wa mwili.<br>2. Chati mguso inayoonesha faida za usafi wa mwili.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada katika Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza faida za usafi wa mwili? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kusafisha mwili wake. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza namna ya kusafisha sehemu za mwili. | 1. Chati/Picha inayoonesha usafishaji wa mwili<br>2. Chati/Picha mguso inayoonesha usafishaji wa mwili. | Je, mwanafunzi anaweza kusafisha mwili wake? | |
| c) Usafi wa Mavazi. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kueleza njia za kutunza mavazi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza njia bora za kutunza mavazi. | 1. Picha zinazoonesha njia mbalimbali za utunzaji wa mavazi.<br>2. Picha mguso zinaoonesha njia mbali mbali za utunzaji wa mavazi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza njia za kutunza mavazi? | **8** |
| | (ii) Kufua mavazi yake.<br>. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kufua nguo zao pamoja na soksi na kung'arisha viatu. | 1. Nguo.<br>2. Pasi ya umeme/mkaa.<br>3. Soksi.<br>4. Sabuni.<br>5. Beseni/Ndoo.<br>6. Maji.<br>7. Viatu.<br>8. Brashi.<br>9. Rangi ya viatu. | Je, mwanafunzi anaweza kufua mavazi yake? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kueleza faida za usafi wa mavazi. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza faida za kusafisha mavazi. | 1. Chati inayoelezea faida za usafi wa mavazi.<br>2. Chati mguso inayoeleza faida za usafi wa mavazi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza faida za usafi wa mavazi? | |
| 2. AFYA YA MWILI.<br>a) Magonjwa ya Kuambukiza. (Surua, Mafua. Kipindupindu. UKIMWI) | Mwanafunzi aweze kutaja magonjwa ya kuambukiza. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza dhana ya magonjwa ya kuambukiza (yaliyoainishwa)<br>2. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | 1. Chati na picha zenye kuonesha magonjwa ya surua, homa ya mafua, kipindupindu na UKIMWI.<br>2. Chati na picha za mguso zenye kuonesha magonjwa ya kuambukiza yaliyotajwa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja magonjwa ya kuambukiza? (yaliyoainishwa) | 6 |
| b) Dalili za Magonjwa ya Kuambukiza. | Mwanafunzi aweze kutaja dalili za magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja dalili za magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | 1. Chati inayoonyesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa)<br>2. Chati mguso inayoonesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | Je, mwanafunzi anaweza kutaja dalili za magonjwa ya kuambukiza? (yaliyoainishwa) | 6 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaeleze wanafunzi dalili za magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | | | |
| c) Njia za Kujikinga na Magonjwa ya Kuambukiza. (yaliyoainishwa) | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza (yaliyoainishwa) | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa)<br>2. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo ya kutaja njia za kujikinga na maradhi ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | 1. Chati inayoonesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa)<br>2. Chati mguso inayoonesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa)<br>3. Kanda za video zinazohusu njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | Je, mwanafunzi anaweza kutaja njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza? (yaliyoainishwa) | **8** |
| | (ii) Kutumia njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza jinsi ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | 1. Chati inayoonesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa)<br>2. Chati mguso inayoonesha magonjwa ya kuambukiza. (yaliyoainishwa) | Je, mwanafunzi anaweza kutumia njia za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza? (yaliyoainishwa) | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. CHAKULA NA LISHE.<br>a) Viini Lishe vya Chakula. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja aina za viini lishe vya chakula. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja viini lishe vya chakula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja viini lishe vya chakula. | 1. Chakula cha uwanga (muhogo, viazi, wali).<br>2. Chakula cha protini (nyama, samaki, maziwa).<br>3. Chakula cha mafuta (siagi, njugu nyasa, samli).<br>4. Chakula cha vitamini (matunda, maziwa, karoti).<br>5. Chakula cha madini (chaza, ngisi, chumvi yenye madini joto). | Je, mwanafunzi anaweza kutaja aina za viini lishe vya chakula? | **6** |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kubainisha vyakula na viini lishe vyake. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha aina ya vyakula na viini lishe vyake. | 1. Chakula cha uwanga (muhogo, viazi, wali).<br>2. Chakula cha protini (nyama, samaki, maziwa).<br>3. Chakula cha mafuta (siagi, njugu nyasa samli).<br>4. Chakula cha vitamini (matunda, maziwa, karoti).<br>5. Chakula cha madini (chaza, ngisi, chumvi yenye madini joto). | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha vyakula na viini lishe vyake? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Usafi na Usalama wa Vyakula. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza umuhimu wa usafi na usalama wa chakula. | 1. Kwa kutumia mbinu ya chemsha bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa usafi na usalama wa chakula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo ya umuhimu wa usafi na usalama wa chakula. | 1. Picha zinazoonesha usalama wa vyakula.<br>2. Picha zinazoonesha usafishaji wa vyombo vya kupikia.<br>3. Picha mguso zinaoonesha usalama wa vyakula.<br>4. Picha mguso zinaoonesha usafishaji wa vyombo vya kupikia. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza umuhimu wa usafi na usalama wa chakula? | **6** |
| | (ii) Kueleza misingi ya usafi na usalama wa chakula. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza misingi ya usafi na usalama wa chakula. | 1. Chati inayoonesha misingi ya usafi na usalama wa chakula.<br>2. Chati mguso inayoonesha misingi ya usafi na usalama wa chakula.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza misingi ya usafi na usalama wa chakula? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kudumisha usafi na usalama wa chakula. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mbinu za kutunza usafi na usalama wa chakula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza jinsi ya kudumisha usafi na usalama wa chakula. | 1. Picha zinazoonesha mbinu za usafi na usalama wa chakula (mfano, kukosha, kufunika na kupasha moto).<br>2. Picha mguso zinaoonesha mbinu za usafi na usalama wa chakula. | Je, mwanafunzi anaweza kudumisha usafi na usalama wa chakula? | |
| 4. HUDUMA YA KWANZA.<br>Huduma ya Kwanza kwa Aliyejikwaruza/ Aliyechubuka. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kueleza jinsi ya kumpa huduma ya kwanza mtu aliyejikwaruza au aliyechubuka. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza namna ya kumpa huduma ya kwanza mtu aliyejikwaruza au aliyechubuka. | 1. Barafu.<br>2. Taulo.<br>3. Kitambaa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza jinsi ya kumpa huduma ya kwanza mtu aliyejikwaruza au aliyechubuka? | **6** |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyejikwaruza/ aliyechubuka. | 1. Kwa kutumia chati, mwalimu awaongoze wanafunzi hatua za kutoa huduma ya kwanza.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo, mwalimu awaoneshe wanafunzi kuigiza namna ya kumpa huduma ya kwanza mtu aliyejikwaruza au aliyechubuka. | 1. Chati inayoonesha utoaji wa huduma ya kwanza kwa mtu aliyejikwaruza/aliyechubuka.<br>2. Chati mguso inayoonesha utoaji wa huduma ya kwanza kwa mtu aliyejikwaruza/aliyejichubua.<br>3. Kisanduku kamilifu.cha huduma ya kwanza<br>4. Kanda za video/CDs/DVD zinazohusu kutoa huduma kwa mtu aliyejikwaruza/ aliyechubuka. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyejikwaruza/ aliyechubuka? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. WANYAMA<br>a) Wanyama Wanaofugwa na Wasiofungwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja wanyama wanaofugwa. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja wanyama wanaofugwa. | 1. Chati zinazoonesha wanyama wanaofugwa.<br>2. Chati mguso zinazoonesha wanyama wanaofugwa.<br>3. Kanda za video zenye wanyama wanaofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja wanyama wanaofugwa? | 8 |
| | (ii) Kutaja wanyama wasiofugwa. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja wanyama wasiofugwa | 1. Chati zinazoonesha wanyama wasiofugwa.<br>2. Chati mguso zinazoonesha wanyama wasiofugwa.<br>3.Kanda za video zenye wanyama wasiofugwa | Je, mwanafunzi anaweza kutaja wanyama wasiofugwa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kuchora baadhi ya wanyama wanaofugwa na wasiofugwa. | Kwa kutumia mbinu ya kuchora, mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora baadhi ya wanyama wanaofugwa na wasiofugwa. | 1. Chati inayoonesha wanyama wanaofugwa ( mbuzi, mbwa, ng’ombe, kondoo, paka)<br><br>2. Chati ya wanyama wasiofugwa (simba, nyoka, paa, chui, twiga).<br><br>3. Chati mguso inayoonesha wanyama wanaofugwa.<br><br>4. Chati mguso inayoonesha wanyama wasiofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza:<br>1. Kuchora picha za wanyama wanaofugwa?<br>2. Kuchora picha za wanyama wasiofugwa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Tabia za Wanyama Wanaofugwa na Wasiofugwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza tabia za wanyama wanaofungwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja tabia za wanyama wanaofugwa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchoro elekezi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja tabia za wanyama wanaofugwa. | 1. Chati ya mchoro elekezi inayoonesha tabia za wanyama wanaofugwa<br>2. Chati mguso elekezi inayoonesha tabia za wanyama wanaofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza tabia za wanyama wanaofugwa? | **4** |
| | (ii) Kueleza tabia za wanyama wasiofugwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja tabia za wanyama wasiofungwa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchoro elekezi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja tabia za wanyama wasiofugwa. | 1. Chati ya mchoro elekezi inayoonesha tabia ya wanyama wasiofugwa.<br>2. Chati mguso ya mchoro elekezi inayoonesha tabia za wanyama wasiofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza tabia za wanyama wasiofugwa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Vyakula vya Wanyama Wanaofugwa na Wasiofugwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja vyakula vya wanyama wanaofugwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya ziara, mwalimu awapeleke wanafunzi sehemu zenye wanyama wanaofugwa ili kuona hali halisi ya vyakula wanavyokula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi vidogo vidogo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vyakula vya wanyama wanaofugwa. | 1. Chati ya vyakula vya wanyama wanaofugwa.<br>2. Chati/Picha mguso ya vyakula vya wanyama wanaofugwa.<br>3. Vyakula halisi vya wanyama wanaofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vyakula vya wanyama wanaofugwa? | **6** |
| | (ii) Kutaja vyakula vya wanyama wasiofugwa. | 1. Kwa kutumia mbinu za ziara mwalimu awapeleke wanafunzi sehemu zenye wanyama wasiofugwa ili kuona hali halisi ya vyakula wanavyokula.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi vidogo vidogo, mwalimu awaongoze wanafunzi kujadiliana juu ya vyakula vya wanyama wasiofugwa. | 1. Chati ya vyakula vya wanyama wasiofugwa.<br>2. Chati/Picha mguso ya vyakula vya wanyama wasiofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vyakula vya wanyama wasiofugwa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. NDEGE<br>a) Ndege Wanaofugwa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuorodhesha ndege wanaofugwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba kuhusu ndege wanaofugwa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha ndege wanaofugwa. | 1. Chati inayoonesha ndege mbalimbali wanaofugwa (kuku, bata, kanga, njiwa, bata mzinga)<br>2. Picha za aina ya ndege mbalimbali wanaofugwa.<br>3. Chati na picha mguso zinaoonesha ndege wanaofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha ndege wanaofugwa? | **6** |
| | (ii) Kuchora baadhi ya ndege wanaofugwa. | Kwa kutumia mbinu ya kuchora, mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora baadhi ya ndege wanaofugwa. | 1. Chati/Picha inayoonesha ndege mbali mbali wanaofugwa.<br>2. Chati/picha mguso inayoonesha ndege mbali mbali wanaofugwa. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora picha za baadhi ya ndege wanaofugwa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Vyakula vya Ndege Wanaofugwa. | Mwanafunzi aweze kuainisha vyakula vya ndege wanaofugwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kujisomea, mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma vitabu vya kiada kuhusu vyakula vya ndege.<br>2. Kwa kutumia njia ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha vyakula vya ndege wanaofugwa. | 1. Nafaka mbalimbali (mtama, mchele, ngano).<br>2. Wadudu mbali mbali.<br>3. Chicha.<br>4. Vitabu vya kiada.<br>5. Vitabu vya kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuainisha vyakula vya ndege wanaofugwa? | **4** |
| 7. WADUDU<br>Aina za Wadudu | Mwanafunzi aweze<br>(i) Kutaja aina za wadudu. | Mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya wadudu mbali mbali katika mazingira yao na kisha wataje majina na aina zao. | 1.Wadudu mbalimbali (vipepeo, panzi, mende, mbu, nzi)<br>2. Kanda za video zinazohusu aina za wadudu. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja aina za wadudu? | **4** |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutaja mifano ya wadudu kutoka kila aina/kikundi. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mifano ya wadudu aina mbalimbali. | 1. Chati inayoonesha wadudu mbalimbali (nyuki, mende, nzi, mbu, kipepeo)<br>2. Wadudu halisi.<br>3. Chati mguso inayoonesha wadudu mbali mbali. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mifano ya wadudu wa aina au makundi mbalimbali? | |
| 8. MIMEA<br>a) Aina za Mimea. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja aina za mimea. | Mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya mimea mbali mbali katika mazingira yao na kisha wataje majina na aina zao. | 1. Mimea halisi.<br>2. Chati ya mimea mbalimbali.<br>3. Chati mguso ya mimea mbali mbali. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja aina za mimea? | **6** |
| | (ii) Kuchora picha za mimea. | Kwa kutumia mbinu ya kuchora mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora mimea. | 1. Mimea halisi.<br>2. Chati ya mimea mbalimbali.<br>3. Chati mguso ya mimea mbali mbali. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora picha za mimea? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Sifa za Mimea. | Mwanafunzi aweze kueleza sifa za mimea. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kujisomea maktaba, mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya taarifa juu ya sifa za mimea.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sifa za mimea. | 1. Mimea halisi<br>2. Chati ya mimea mbalimbali.<br>3. Chati mguso ya mimea mbali mbali.<br>4. Vitabu vinavyoeleza sifa za mimea.<br>5. Vitabu vya Braille vinavyoeleza sifa za mimea. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sifa za mimea? | **4** |
| 9. MAJI.<br>a) Vyanzo vya Maji. | Mwanafunzi aweze kutaja vyanzo vya maji. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vyanzo mbalimbali vya maji. | 1.. Picha za vyanzo vya maji.<br>2. Picha mguso za vyanzo vya maji.<br>3. Vyanzo halisi vya maji.<br>4. Kanda za video zinazohusu vyanzo vya maji. | Je, mwanafnzi anaweza kutaja vyanzo vya maji? | 4 |
| b) Umuhimu wa Maji. | Mwanafunzi aweze kueleza umuhimu wa maji. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa maji. | 1. Chati. inayoonesha umuhimu wa maji katika maisha ya kila siku ya binadamu.<br>2. Picha mguso inayoonesha umuhimu wa maji katika maisha ya kila siku ya binadamu. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza umuhimu wa maji? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Matumizi ya Maji. | Mwanafunzi aweze kutaja matumizi ya maji. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo kuhusu matumizi ya maji.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja matumizi ya maji. | 1. Chati inayoonesha matumizi ya maji (kufua,kumwagilia mimea, kunywa, kupika, kuoga).<br>2. Chati mguso inayoonesha matumizi ya maji.<br>3. Kanda za video/ CDs/DVD zinazohusu matumizi ya maji. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja matumizi ya maji? | 4 |
| 10. HEWA.<br>a) Vyanzo vya Hewa. | Mwanafunzi aweze kueleza sehemu inazopatikana hewa. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sehemu inazopatikana hewa. | 1. Chupa.<br>2. Maji.<br>3. Udongo.<br>4. Vikopo. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sehemu inazopatikana hewa? | 4 |
| b) Umuhimu wa Hewa. | Mwanafunzi aweze kueleza umuhimu wa hewa kwa viumbe hai. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa hewa kwa viumbe hai. | 1. Chati inayoonesha umuhimu wa hewa kwa viumbe hai.<br>2. Chati mguso inayoonesha umuhimu wa hewa kwa viumbe hai. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza umuhimu wa hewa kwa viumbe hai? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Matumizi ya Hewa. | Mwanafunzi aweze kutaja matumizi ya hewa. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja matumizi ya hewa. | 1. Chati inayoonesha matumizi mbalimbali ya hewa.<br>2. Chati mguso inayoonesha matumizi mbali mbali ya hewa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja matumizi ya hewa? | 4 |
| 11. MWANGA.<br>a) Vyanzo vya Mwanga Asili. | Mwanafunzi aweze kutaja vyanzo vya mwanga asili. | Kwa kutumia mbinu ya kujisomea, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vyanzo vya mwanga asili. | 1. Chati inayoonesha vyanzo vya mwanga asili (jua na nyota).<br>2. Kitabu cha kiada.<br>3. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille.<br>4. Chati mguso inayoonesha vyanzo vya mwanga asili. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vyanzo vya mwanga asili? | 4 |
| b) Vyanzo vya Mwanga Visivyo Asili. | Mwanafunzi aweze kutaja vyanzo vya mwanga visivyo asili. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vyanzo vya mwanga visivyo asili. | 1.Chati inayoonyesha vyanzo vya mwanga visivyo asili (tochi, kibatari, kandili, mshumaa).<br>2. Chati mguso inayoonesha vyanzo vya mwanga visivyo asili. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vyanzo vya mwanga visivyo asili? | 4 |

| MADA KUU / MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 12. SAUTI<br>Vyanzo vya Sauti. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja vitu vinavyotoa sauti. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vitu vinavyotoa sauti. | Vitu vinavyotoa sauti (kengele, mabati, ngoma, filimbi). | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vitu vinavyotoa sauti? | 6 |
| | (ii) Kuonesha jinsi ya kupata sauti. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaoneshe wanafunzi jinsi ya kupata sauti kutoka kwenye vitu tofauti. | Vitu vinavyotoa sauti (kengele, mabati, ngoma, filimbi). | Je, mwanafunzi anaweza kuonesha jinsi ya kupata sauti kutoka vitu mbali mbali? | |
| 13. JOTO<br>Vyanzo vya Joto Asili. | Mwanafunzi aweze kutaja vitu vinavyotoa joto asili. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vitu vinavyotoa joto asili.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vitu vinavyotoa joto asili. | Vitu vinavyotoa joto asili (moto, jua). | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vitu vinavyotoa joto asili? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 14. UMEME.<br>Vyanzo vya Umeme. | Mwanafunzi aweze kutaja vitu vinavyotoa umeme. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vitu vinavyotoa umeme. | 1. Betri.<br>2. Maporomoko ya maji.<br>3. Nuru ya jua.<br>4. Upepo.<br>5. Kinu cha baiskeli.<br>6. Genereta. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vitu vinavyotoa umeme? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kupiga na kupokea simu ya mezani. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kupiga na kupokea simu ya mezani.<br>2. Kwa kutumia ya mzoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kupiga na kupokea simu ya mezani. | Simu ya mezani. | Je, mwanafunzi anaweza kupiga na kupokea simu ya mezani? | |
| 17 MAKTABA<br>Maktaba na Matumizi Yake. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya maktaba. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya maktaba. | 1. Picha ya maktaba.<br>2. Picha mguso ya maktaba.<br>3. Maktaba halisi | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya maktaba? | 4 |
